Jedwali Na. 24. 5: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, SMT 2022 .....	293
Jedwali Na. 24. 6: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Busega, SMT 2022.....	294
Jedwali Na. 0 25.0: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Halmashauri; Mkoa wa Geita, SMT 2022.....	295
Jedwali Na. 25. 1: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Geita, SMT 2022.....	295
Jedwali Na. 25. 2: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Mji wa Geita, SMT 2022.....	296
Jedwali Na. 25. 3: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Nyang'hwale SMT 2022 .....	297
Jedwali Na. 25. 4: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Mbogwe SMT 2022.....	297
Jedwali Na. 25. 5: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, SMT 2022 .....	298
Jedwali Na. 25. 6: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Chato, SMT 2022.....	299
Jedwali Na. 26.0: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Halmashauri; Mkoa wa Songwe, SMT 2022.....	300
Jedwali Na. 26. 1: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Momba, SMT 2022 .....	300

<b>Jedwali Na. 26. 2: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Mji wa Tunduma, SMT 2022.....</b>	<b>301</b>
<b>Jedwali Na. 26. 3: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, SMT 2022 .....</b>	<b>301</b>
<b>Jedwali Na. 26. 4: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, SMT 2022.....</b>	<b>302</b>
<b>Jedwali Na. 26. 5: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Kata; Halmashauri ya Wilaya ya Illeje, SMT 2022.....</b>	<b>303</b>
<b>Jedwali Na. 27.0: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Baraza; Mkoa wa Kaskazini Unguja, SMT 2022.....</b>	<b>304</b>
<b>Jedwali Na.27. 1: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Manispaa Kaskazini A, SMT 2022.....</b>	<b>304</b>
<b>Jedwali Na.27. 2: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Mji Kaskazini B, SMT 2022 .....</b>	<b>305</b>
<b>Jedwali Na. 0 28.0: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Halmashauri; Mkoa wa Kusini Unguja, SMT 2022.....</b>	<b>307</b>
<b>Jedwali Na. 28. 1: Idadi ya Majengo kwa Aina, Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Mji Kati, SMT 2022 .....</b>	<b>307</b>
<b>Jedwali Na. 28. 2: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, SMT 2022.....</b>	<b>308</b>
<b>Jedwali Na. 0 29: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Baraza; Mkoa wa Mjini Magharibi, SMT 2022.....</b>	<b>310</b>

<b>Jedwali Na. 29. 1: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Manispaa Mjini, SMT 2022.....</b>	<b>310</b>
<b>Jedwali Na. 29. 2: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Manispaa Magharibi A, SMT 2022 .....</b>	<b>312</b>
<b>Jedwali Na. 29. 3: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Manispaa Magharibi B, SMT 2022 .....</b>	<b>313</b>
<b>Jedwali Na. 30.0: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Halmashauri/Baraza; Mkoa wa Kaskazini Pemba, SMT 2022 .....</b>	<b>314</b>
<b>Jedwali Na. 30. 1: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Mji Wilaya ya Wete, SMT 2022 .....</b>	<b>314</b>
<b>Jedwali Na. 30. 2: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, SMT 2022 .....</b>	<b>315</b>
<b>Jedwali Na. 0 31.0: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Baraza; Mkoa wa Kusini Pemba, SMT 2022 .....</b>	<b>317</b>
<b>Jedwali Na. 31. 1: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Manispaa Chakechake, SMT 2022.....</b>	<b>317</b>
<b>Jedwali Na. 31. 2: Idadi ya Majengo Kwa Aina na Matumizi Makuu na Shehia; Baraza la Mji Mkoani, SMT 2022.....</b>	<b>318</b>

## **Orodha ya Ramani**

Ramani Na. 2.1: Idadi ya Majengo kwa Mikoa; Tanzania, SMT 2022.....	49
---	----



## Dhana na Tafsiri

### Anwani ya Makazi

Ni miundombinu inayotambulisha mahali jengo mahali kupitia namba na jina la mtaa au barabara.

### Hati ya Ardhi

Hii ni nyaraka ya kisheria ya umiliki wa ardhi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 ya Tanzania Bara na Sheria ya Umiliki wa Ardhi Namba 12 ya mwaka 1992 ya Tanzania Zanzibar.

### Hati ya Kimila ya Umiliki wa Ardhi

Hii ni nyaraka ya kisheria ya umiliki wa ardhi inayotolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya 1999.

### Jengo

Ni tokeo la kudumu la kazi ya binadamu lenye kuhusisha ujenzi wa kuta, paa, na sakafu; kwa kusudi la kuleta kinga kwa binadamu juu ya hali ya hewa na majanga, kuleta mahali salama pa kuishi, kupata faragha, kutunza vitu vya thamani au wanyama na mahali pa kazi.

### Jengo liliilo peke yake

Nyumba/jengo liliyojengwa peke yake kuanzia msingi hadi paa bila kuungana na nyingine. Jengo linaweza kuwa la ghorofa au lisilo la ghorofa.

### Jengo halifai kwa matumizi

Jengo hatarishi kwa matumizi ya binadamu au kuhifadhi bidhaa (lililochakaa, linalokaribia kuanguka au lenye nyufa kubwa kwenye kuta).

### Jengo la muda

Jengo ambalo kwa jinsi lilivyo haliwezi kudumu bila kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara. Majengo haya yamejengwa kwa vifaa visivyo vya kudumu kama vile nyasi, makuti, matete au udongo.

### Leseni za Makazi

### Maeneo yaliyopimwa

### Majengo yasiyo ya makazi

Haya ni majengo yanayotumika kwa matumizi yasiyo ya makazi kama vile majengo ya biashara pekee (mf. maduka), ofisi, huduma za kijamii (mf. shule, hospitali, vituo vya polisi), majengo ya ibada, viwanda au maghala ya kuhifadhia bidhaa na vyakula na mengineyo yanayofanana na hayo.

<b>Safu ya majengo yaliyoungana</b>	Jengo lenye msururu wa majengo zaidi ya mawili yaliyoungana yenyepaa moja. Jengo linaweza kuwa la ghorofa au lisilo la ghorofa.
<b>Sehemu ya Jengo imekamilika</b>	Jengo ambalo sehemu ya jengo iimekamilika na iinatumika na sehemu nyingine haijakamilika kwa maana ujenzi unaendelea.
<b>Sensa ya Majengo</b>	Ni zoezi la ukusanyaji, uchakataji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa zinazohusu majengo kwa kipindi maalum.
<b>Uniti</b>	Nyumba au sehemu ya jengo ambalo lina matumizi kamili (kula, kulala na sebule). Jengo moja linaweza kuwa na uniti moja au zaidi.

## Dibaji



Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya Sensa ya Majengo Tanzania (SMT) mwaka 2022 ambayo ni ya kwanza kufanyika nchini. Aidha ni sensa ya kwanza ya Majengo kufanyika kwa kina katika ukanda wa Afrika Mashariki. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa



Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Serikali ya Awamu ya Nane chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wametimiza wajibu wao wa kuendesha Sensa ya Majengo Tanzania ya mwaka 2022 (SMT, 2022). Hatua hii, mbali na kutatua changamoto za muda mrefu za ukosefu wa taarifa za majengo nchini, imekidhi matakwa ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na programu mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazohusiana na Maendeleo ya Makazi ya Watu. Hivyo, tunawiwa kutoa shukrani nyingi kwa kujitolea kwao na kwa msaada wao usioyumba katika kipindi chote cha mchakato wa utekelezaji wa Sensa ya Majengo Tanzania, 2022 .

Kwa kuzingatia uhusiano uliopo kati ya majengo na idadi ya watu, kufanyika kwa Sensa ya Kwanza ya Majengo ya mwaka 2022 kumetekeleza Sheria ya Takwimu Sura ya 351 inayoipa mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi. Kwa muktadha huu, inamaanisha kuwa, Sensa ya Majengo na Sensa ya Watu na Makazi zinaweza kuoanishwa. Uamuzi wa Serikali wa kutumia teknolojia ya hali ya juu katika mchakato mzima wa utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 na SMT, 2022, umeifanya sensa hii ya kwanza ya Majengo kuwa ya kidijitali nchini Tanzania.

Kwa ujumla, matokeo ya SMT ya mwaka 2022, ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi yakitarajiwa kuleta athari chanya katika makundi makuu ya matumizi ya majengo ambayo ni makazi, biashara, viwanda na taasisi. Takwimu za sensa ya majengo pamoja na uhuishaji wake wa mara kwa mara utasaidia katika kuongeza uelewa na uwazi katika kugawa rasilimali zinazohitajika kwa maendeleo ya majengo katika ngazi zote za utawala kulingana na mahitaji halisi.

Kwa kuzingatia hali ya maendeleo ya makazi ya watu mijini na vijijini, matokeo ya SMT, 2022, yatatumiwa na Serikali pamoja na wadau wengine katika ufuatiliaji na tathmini ya mifumo mbalimbali ya maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo; Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025; Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2021/22 - 2025/26; Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2050; na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063. Matokeo pia yatatoa takwimu ambazo zitaiwezesha Serikali kutathmini utekelezaji wa Lengo

Namba 11 la Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030, linalolenga kuweka miji na makazi ya binadamu kuwa jumuishi, salama, imara na endelevu.

Lengo kuu la ripoti hii ni kutoa taarifa za kina za majengo zinazotokana na Sensa ya Majengo ya mwaka 2022, ikiwa na pamoja na idadi ya majengo, sifa za jengo,, upatikanaji wa huduma muhimu katika jengo na hali ya umiliki. Taarifa za uchambuzi katika ripoti hii, zimewasilishwa katika ngazi ya taifa na mkoa. Hata hivyo, taarifa kuhusu idadi na aina ya majengo na matumizi zinapatikana hadi ngazi ya Kata/Shehia.

Kukamilika kwa SMT ya mwaka 2022 kulitokana wa ushirikiano kutoka Serikalini kupitia Kamati za Sensa kuanzia ngazi za juu hadi za chini za kiutawala. Hizi ni pamoja na Kamati Kuu ya Taifa ya Sensa inayojumuisha Mawaziri wa Kisekta; Kamati ya Ushauri ya Sensa ya Taifa inayojumuisha Makatibu Wakuu wa Kisekta; Kamati ya Ufundu ya Sensa ya Taifa; Kamati za Sensa katika Mikoa, Wilaya, Kata/Shehia, Kijiji/Mtaa na Vitongoji; na, Vikao kutoka kwa Watendaji Wasio wa kiserikali ikiwa ni pamoja na Sekta Binafsi, Taasisi mbalimbali na Umma kwa ujumla. Tunawashukuru kwa ushirikiano wao mkubwa.

Shukrani za pekee zinatolewa kwa Washirika wa Maendeleo wafuatao:- Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA); Benki ya Dunia (WB); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF); UN-Wanawake; Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM); Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID); Ofisi ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo (FCDO); Ofisi ya Sensa ya Marekani (USCB), Jamhuri ya Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China na Washirika wengine wa Maendeleo kwa kutoa vifaa, utaalamu, mafunzo na msaada wa kifedha katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi pamoja na Sensa ya Majengo ya 2022. Pia tunawashukuru viongozi wa dini, kimila na kisiasa, viongozi wa asasi zisizo za kiserikali, vyombo vyaa habari na wananchi wote na wasio raia kwa ujumla kwa ushiriki na michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa Sensa hizi.

Aidha tunawashukuru waheshimiwa Anne Semamba Makinda - Kamisaa wa Sensa Tanzania Bara na Spika wa zamani wa Bunge; na Mheshimiwa Balozi Mohamed Haji Hamza - Kamisaa wa Sensa Tanzania Zanzibar, kwa uongozi na usimamizi wao madhubuti katika kuelimisha na kuhamasisha wananchi kushiriki katika Sensa hizi. Pia tunamshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Dk Amina Msengwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Takwimu Zanzibar Balozi Amina Salum Ali kwa miongozo yao katika kipindi chote cha utekelezaji wa zoezi la Sensa.

Mwisho kabisa, tunapenda kutambua juhudu na dhamira isiyo na kifani ya Menejimenti na wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu chini ya uongozi wa Dk. Albina Chuwa, Mtakwimu Mkoo; na wafanyakazi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkoo wa Serikali, Zanzibar chini ya uongozi wa Mheshimiwa Salum Kassim Ali; Mtakwimu Mkoo wa Serikali; watumishi kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; pamoja na maofisa wengine wa Serikali

waliofanya kazi bila kuchoka katika kuhakikisha kuwa sensa hizi za Majengo pamoja na Watu na Makazi ya mwaka 2022 zinatekelezwa kwa mafanikio makubwa.



**Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**  
Waziri Mkuu wa  
Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania.



**Hemed Suleiman Abdulla (MBM)**  
Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali  
ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Shukrani

Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkoo wa Serikali, Zanzibar zilifanya Sensa ya Majengo Tanzania (SMT) ya mwaka 2022 kwa lengo la kuwa na taarifa muhimu za kufanya mapitio na uandaaji wa sera, upangaji wa miradi, ufuatiliaji na tathmini ya mchakato wa uendelezaji wa makazi ya watu nchini. Sensa ya Majengo ya mwaka 2022 ilikusanya taarifa za kina kuhusu majengo zinazojumuisha kwa upana aina za majengo, sifa za majengo, upatikanaji wa huduma muhimu katika jengo na hali ya umiliki wa jengo.

Kutokana na mafanikio haya tunapenda hasa kutoa shukrani zetu kwa watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Maakazi Zanzibar, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkoo wa Serikali, Zanzibar (OCGS), ambao walifanya kazi kwa juhudini katika kuhakikisha kuwa Sensa ya Majengo ya 2022 inatekelezwa kwa ufanisi.

Shukrani zetu pia ziwaendee wataalamu wote, wasimamizi wa Mikoa na Wilaya, wajumbe na wasimamizi pamoja na vyombo vya habari kwa kazi yao nzuri. Hakika, bila kujituma na na kujitoa kwao, Sensa hii ya Majengo isingefanikiwa. Tunapenda pia kuwashukuru wananchi kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha zoezi la kitaifa la Sensa ya Majengo.

Aidha, tunathamini sana michango yote iliyotolewa na Wadau wa Maendeleo pamoja na Taasisi za Umma na Binafsi, makundi mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini, kimila kisiasa, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za watu wenye ulemavu na wengine wote wenye waliochangia mafanikio ya SMT, 2022. Matokeo ya mafanikio haya yamewezesha kupatikana kwa Ripoti hii ya SMT ambayo itatoa takwimu zenye uhakika kwa maendeleo endelevu ya makazi ya watu kijamii na kiuchumi nchini.



**Dr. Albina Chuwa**

Mtakwimu Mkoo wa Serikali  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu



**Salum Kassim Ali**

Mtakwimu Mkoo wa Serikali,  
Ofisi ya Mtakwimu Mkoo wa Serikali,  
Zanzibar

## Muhtasari

Sensa ya Majengo Tanzania ya Mwaka 2022 (SMT, 2022), ilifanyika ili kukabiliana na changamoto za muda mrefu za ukosefu wa taarifa za majengo nchini pamoja na kukidhi matakwa ya sera mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazohusu maendeleo ya makazi ya watu. Taarifa zilizokusanywa ni pamoja na idadi ya majengo yote nchini, aina ya majengo, matumizi ya majengo, ubora wa majengo, umiliki wa majengo kwa kuzingatia jinsi, sifa za majengo na hali ya upimaji wa ardhi ambapo majengo yamejengwa.

**Sura ya kwanza** inawasilisha taarifa fupi ikiwemo usuli, mantiki na malengo ya kufanya Sensa ya Majengo Tanzania ya Mwaka 2022 (SMT 2022). Serikali ilifanya kwa mara ya kwanza sensa ya majengo mwaka 2022, zoezi lilofanyika sanjari na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 SMT ilizingatia kifungu cha 4.1.8.2 (ii) cha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na Kifungu cha 5.4.11 cha Sera ya Taifa ya Ardhi ya Zanzibar 2018 pamoja na Kifungu cha 2.5 cha Sera ya Taifa ya Nyumba ya Mwaka 2008 ya Zanzibar. Lengo kuu la SMT 2022 ni kulipatia taifa takwimu za kutosha na za uhakika za majengo ili kuimarisha maamuzi yanayozingatia ushahidi katika ngazi zote za utawala kwa maendeleo endelevu ya makazi ya watu.

**Sura ya pili** inawasilisha taarifa kuhusu idadi ya majengo. Matokeo yanaonesha kuwa idadi ya majengo yote Tanzania ni 14,348,372 ambapo 13,907,951 yapo Tanzania Bara na majengo 440,421 yapo Tanzania Zanzibar. Aidha majengo mengi (asilimia 94.4) Tanzania siyo ya ghorofa. Majengo tisa kati ya kumi ni kwa ajili ya makazi na asilimia 3.4 ni ya biashara-makazi. Kwa upande mwingine, asilimia 98.0 ya majengo yote ya makazi na biashara-makazi ni ya uniti moja.

**Sura ya tatu** inawasilisha taarifa kuhusu hali ya ujenzi, hali ya ukaazi, vifaa vya ujenzi, idadi ya vyumba vya kulala na hali ya jengo. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 94.3 ya majengo yote Tanzania ni jengo moja moja (stand-alone). Matokeo yanaonesha pia kuwa asilimia 71.7 ya majengo yote nchini ujenzi wake umekamilika. Zaidi ya majengo manne kati ya kumi yana sakafu ya saruji au vigae, au marumaru ambapo asilimia 77.7 yameezekwa kwa mabati. Asilimia 58.7 ya majengo yote ya makazi na

ya biashara-makazi yana chumba kimoja au viwili vya kulala. Aidha, asilimia 12.8 ya majengo yote Tanzania yanahitaji ukarabati mkubwa.

**Sura ya nne** inawasilisha taarifa kuhusu huduma za msingi katika jengo zilizokusanywa katika Sensa ya Majengo Tanzania ya mwaka 2022. Huduma hizo zimegawanyika katika sehemu kuu mbili; huduma katika jengo (umeme, maji na choo); na hali ya kufikika kwa jengo (barabara) na uwepo wa miundombinu ya watu wenyе ulemavu. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 23.4 ya majengo yote Tanzania yanapata umeme kutoka gridi ya Taifa na asilimia 28.2 yanatumia vyanzo mbadala vya umeme. Majengo yenyе huduma ya maji ni asilimia 24.9 ambapo asilimia 77.5 yana huduma ya vyoo. Kwa upande mwingine, asilimia 72.6 ya majengo yote yanafikika kwa barabara ambapo asilimia 3.9 pekee ndiyo yenyе miundombinu ya Watu Wenye Ulemavu.

**Sura ya tano** inawasilisha taarifa kuhusu umiliki na hali ya umiliki wa majengo, hali ya upimaji wa ardhi pamoja na uwepo wa nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi lilipojengwa jengo. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 87.0 ya majengo yote Tanzania yanamilikiwa na watu binafsi. Kati ya majengo yote yanayomilikiwa na mtu mmoja mmoja, wanaume wanamiliki takribani mara tatu (71.5%) ukilinganisha na majengo yanayomilikiwa na wanawake (23.4%) ambapo asilimia 5.1 yanamilikiwa kwa pamoja. Takriban theluthi mbili (67.1%) ya majengo yote Tanzania yamejengwa kwenye ardhi ambayo haijapimwa ambapo asilimia 33.3 hayana nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi.

**Sura ya sita** inawasilisha matokeo muhimu, tafsiri za kisera na mapendekezo.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Matokeo ya Sensa ya Majengo: Tanzania**

\\Kiashiria	Tanzania		Tanzania Vijijini		Tanzania Mjini		Tanzania Bara		Tanzania Zanzibar	
	Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia	Jumla	Asilimia
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>70.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>30.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>96.9</b>	<b>440,421</b>	<b>3.1</b>
<b>Idadi ya Majengo Kwa Anwani ya Makazi</b>										
Majengo yenyne Anwani ya Makazi	10,751,123	74.9	7,546,377	75.2	3,204,746	74.4	10,406,722	74.8	344,398	78.2
Majengo yasiyo na Anwani ya Makazi	3,597,249	25.1	2,491,824	24.8	1,105,425	25.6	3,501,306	25.2	96,023	21.8
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>100.0</b>	<b>440,421</b>	<b>100.0</b>
<b>Idadi ya Majengo kwa Aina ya Jengo</b>										
Ghorofa	68,724	0.5	11,131	0.1	57,593	1.3	61,258	0.4	7,466	1.7
Nyumba isiyo ya ghorofa	13,540,363	94.4	9,558,456	95.2	3,981,907	92.4	13,152,298	94.6	388,065	88.1
Aina nyingine kihatua (Msingi)	739,285	5.2	468,614	4.7	270,671	6.3	694,395	5.0	44,890	10.2
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>100.0</b>	<b>440,421</b>	<b>100.0</b>
<b>Idadi ya Majengo kwa Matumizi Makuu ya Jengo</b>										
Makazi	13,112,235	91.4	9,307,250	92.7	3,804,985	88.3	12,717,893	91.4	394,342	89.5
Makazi na Biashara	493,093	3.4	242,259	2.4	250,834	5.8	470,476	3.4	22,617	5.1
Matumizi yasiyo ya Makazi	743,044	5.2	488,692	4.9	254,352	5.9	719,582	5.2	23,462	5.3
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>100.0</b>	<b>440,421</b>	<b>100.0</b>
<b>Idadi ya Majengo kwa Hali ya Ujenzi wa Jengo</b>										
Jengo limekamilika	10,284,090	71.7	7,311,301	72.8	2,972,789	69.0	10,056,349	72.3	227,741	51.7
Sehemu ya jengo imekamilika	1,194,391	8.3	786,236	7.8	408,155	9.5	1,124,460	8.1	69,931	15.9
Jengo linaendelea kujengwa	2,062,874	14.4	1,261,154	12.6	801,720	18.6	1,936,847	13.9	126,027	28.6
Jengo la muda	807,017	5.6	679,510	6.8	127,507	3.0	790,295	5.7	16,722	3.8
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>100.0</b>	<b>440,421</b>	<b>100.0</b>
<b>Idadi ya Majengo kwa Hali ya Ukaazi</b>										
Linatumika	12,445,648	86.7	8,789,426	87.6	3,656,222	84.8	12,096,768	87.0	348,880	79.2
Halitumiki	1,902,724	13.3	1,248,775	12.4	653,949	15.2	1,811,183	13.0	91,541	20.8
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>	<b>13,907,951</b>	<b>100.0</b>	<b>440,421</b>	<b>100.0</b>

<b>Idadi ya Majengo kwa Huduma za Msingi</b>										
Umeme wa Gridi ya Taifa (TANESCO/ZECO)	3,354,146	23.4	1,113,541	11.1	2,240,605	52.0	3,134,547	22.5	219,599	49.9
Umeme mwingine (mf. sola, jenereta)	4,048,026	28.2	3,288,967	32.8	759,059	17.6	4,031,401	29.0	16,625	3.8
Maji	3,572,597	24.9	1,520,753	15.1	2,051,844	47.6	3,374,446	24.3	198,151	45.0
Choo	11,120,843	77.5	7,467,381	74.4	3,653,462	84.8	10,806,308	77.7	314,535	71.4
<b>Idadi ya Majengo kwa Huduma Nyengine</b>										
Barabara	10,415,962	72.6	6,830,497	68.0	3,585,465	83.2	10,144,645	72.9	271,317	61.6
Miundombinu ya watu wenye ulemavu	562,056	3.9	318,527	3.2	243,529	5.7	542,020	3.9	20,036	4.5
<b>Idadi ya Majengo kwa Jinsi ya Mmiliki wa Jengo</b>										
Mwanaume	9,827,124	71.5	6,848,747	72.2	2,978,377	70.1	9,719,370	70.6	340,593	77.3
Mwanamke	3,217,943	23.4	2,122,553	22.4	1,095,390	25.8	3,361,900	24.4	87,672	19.9
Mwanaume/wanaume na Mwanamke/wanawake	670,616	4.9	505,971	5.3	164,645	3.9	660,926	4.8	9,690	2.2
Wanaume kwa pamoja	13,929	0.1	8,005	0.1	5,924	0.1	12,252	0.1	1,677	0.4
Wanawake kwa pamoja	7,144	0.1	3,565	0.0	3,579	0.1	6,332	0.0	812	0.2
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,201,224</b>	<b>100.0</b>	<b>9,838,589</b>	<b>100.0</b>	<b>4,362,635</b>	<b>100.0</b>				
<b>Idadi ya Majengo kwa Mtumiaji wa Jengo/Uniti</b>										
Mmiliki	10,252,761	83.3	7,633,947	89.5	2,618,814	69.3	9,968,918	83.4	283,967	81.3
Mtu mwingine bila kulipa kodi	597,033	4.9	404,732	4.7	192,301	5.1	564,689	4.7	32,332	9.3
Mmiliki pamoja na wapangaji	328,249	2.7	88,108	1.0	240,141	6.4	322,224	2.7	6,010	1.7
Wapangaji	1,130,379	9.2	404,231	4.7	726,148	19.2	1,103,399	9.2	26,983	7.7
<b>Idadi ya Majengo ya Makazi na Biashara</b>	<b>12,308,122</b>	<b>100.0</b>	<b>8,530,786</b>	<b>100.0</b>	<b>3,777,336</b>	<b>100.0</b>				
<b>Idadi ya Majengo kwa hali ya Upimaji wa Eneo lilipojengwa Jengo</b>										
Limepimwa	1,553,744	10.8	463,597	4.6	1,090,147	25.3	1,445,924	10.4	108,220	24.6
Halijapimwa	10,428,113	72.7	8,392,470	83.6	2,035,643	47.2	10,202,076	73.3	226,037	51.3
Limerasimishwa	1,899,397	13.2	937,880	9.3	961,517	22.3	1,844,401	13.3	54,996	12.5

Hajui	467,118	3.3	244,254	2.4	222,864	5.2	415,950	3.0	51,168	11.6
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,348,372</b>	<b>100.0</b>	<b>10,038,201</b>	<b>100.0</b>	<b>4,310,171</b>	<b>100.0</b>				
<b>Idadi ya Majengo/Uniti kwa Nyaraka ya Kisheria ya Umiliki</b>										
Hati ya umiliki (Title deed)	1,525,911	10.4	420,644	4.1	1,105,267	24.3	1,422,374	10.0	103,337	22.7
Leseni ya makazi	231,283	1.6	30,996	0.3	200,287	4.4	231,342	1.6	-	-
Barua ya toleo (Ofa)/Ushuhuda wa malipo	601,547	4.1	195,344	1.9	406,203	8.9	585,420	4.1	18,355	4.0
Hatimiliki ya kimila	3,650,990	24.8	3,229,685	31.8	421,305	9.3	3,593,264	25.2	59,936	13.1
Mikataba	540,755	3.7	256,327	2.5	284,428	6.3	526,717	3.7	16,202	3.6
Nyaraka za serikali ya mtaa/kijiji	6,520	0.1	3,132	0.0	3,388	0.1	-	-	8,749	1.9
Hakuna nyaraka ya kisheria	2,420,991	17.5	1,449,126	15.4	971,865	22.2	2,535,417	17.8	38,986	8.5
Hajui	4,750,489	33.3	3,980,335	40.3	470,154	17.7	4,755,238	33.3	148,396	32.5
Hati ya umiliki (Title deed)	526,981	4.6	249,352	3.6	277,629	6.9	618,339	4.3	61,892	13.6
<b>Idadi ya Majengo</b>	<b>14,724,164</b>	<b>100.0</b>	<b>10,167,659</b>	<b>100.0</b>	<b>4,556,505</b>	<b>100.0</b>				

## SURA YA KWANZA

### USULI

#### 1.0 Utangulizi

Majengo ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika maisha ya watu nchini Tanzania na duniani kote, inayosaidia kuhifadhi na kuendeleza maisha ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Matumizi makuu ya majengo katika maisha ya watu wa mijini na vijijini ni pamoja na makazi, biashara, makazi na biashara, taasisi na viwanda. Aidha, ujenzi kama sehemu ya majengo ni kigezo muhimu cha kupima hali ya uchumi usio wa kipato kwa mtu binafsi au jamii husika.

Pamoja na umuhimu mkubwa wa majengo katika maisha ya jamii katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, Tanzania hajawahi kuwa na takwimu za majengo za kutosha, za uhakika na za wakati zinazojumuisha majengo yote nchini. Takwimu za majengo ambazo zimekuwa zikitumika kupanga na kufanya maamuzi katika ngazi mbalimbali za utawala zimekuwa zikipatikana kwa makadirio ya idadi inayohusu aina chache za majengo hasa makazi, elimu na taasisi za afya. Kwa muda mrefu, mapungufu haya yamesababisha Tanzania kukosa kanzidata ya kitaifa ya majengo, rasilimali ambayo ingesaidia katika kuandaa sera, mipango na miradi mbalimbali ya kuleta au kuboresha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika ngazi mbalimbali za utawala nchini.

Ili kuondokana na ukosefu wa takwimu za majengo kitaifa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya kwanza ilifanya Sensa ya Majengo Tanzania mwaka 2022 (SMT, 2022). , Zoezi hili lilifanyika sambamba na Sensa ya Sita ya Watu na Makazi ambayo ilifanyika usiku wa tarehe 22 kuamkia 23 Agosti 2022. Mbali na kukabiliana na changamoto za muda mrefu za ukosefu wa taarifa za majengo nchini, SMT ilifanyika ili kukidhi matakwa ya sera mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa zinazohusu maendeleo ya makazi ya watu. Utekelezaji huu mkubwa wa kitaifa uliweza kufanyika kutokana na uelewa kwamba, sensa ya majengo ni njia ya msingi ya kupata taarifa i za majengo ambazo ni sahihi, za kutosha na kwa wakati.

Ripoti hii ya Sensa ya Majengo Tanzania ya mwaka 2022 ina sura sita ambazo zinatoa majibu ya mada zote zilizoulizwa kwenye Dodoso la Sensa ya Majengo iliyofanyika Mwezi Agosti 2022. Viashiria hivyo ni pamoja na idadi ya majengo yote nchini, aina ya majengo, matumizi ya majengo, ubora wa majengo, umiliki wa majengo kwa kuzingatia jinsi, sifa za majengo na hali ya upimaji wa ardhi ambapo majengo yamejengwa. Ripoti hii inatoa uchambuzi mfupi wa takwimu za majengo kwa ngazi ya

kitaifa na mkoa. Hata hivyo, takwimu za idadi, aina na matumizi ya majengo zimetolewa hadi ngazi ya Kata/Shehia.

Kwa kuzingatia umuhimu wa matokeo ya SMT 2022, matumizi rasmi ya takwimu za sensa katika ofisi za umma na binafsi yanapaswa kuimarishwa na kusimamia ipasavyo ili taifa liweze kufikia malengo yaliyokusudiwa ambayo ni kuleta maendeleo endelevu ya Sekta ya Makazi kijamii na kiuchumi.

### **1.1 Mantiki**

Uamuzi wa kufanya Sensa ya Majengo Tanzania ya mwaka 2022 unazingatia utekelezaji wa Kifungu cha 4.1.8.2 (ii) cha Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Kifungu hiki kinalekeza Serikali kuandaa takwimu za nyumba na makazi zitakazosaidia katika kufanya maamuzi ya maboresho ya kisekta kama vile kukidhi mahitaji ya nyumba na kudhibiti ukuaji wa miji kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, utekelezaji wa SMT 2022 umezingatia Kifungu cha 5.4.11 cha Sera ya Taifa ya Ardhi ya Zanzibar ya mwaka 2018, kinachozitaka taasisi zinazohusika na Takwimu za Kitaifa kukusanya takwimu za ardhi na shughuli zinazohusiana nazo. Kifungu hiki kinalekeza kutoa takwimu na taarifa kwa wadau wote husika watakaosaidia katika mchakato wa upangaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi. Vilevile SMT 2022 imezingatia matakwa ya Kifungu cha 2.5 cha Sera ya Nyumba ya Zanzibar ya mwaka 2008 kinacholenga upatikanaji wa makazi endelevu kwa watu wa ngazi zote za jamii.

Aidha, SMT 2022 ni msingi na chanzo cha uhakika cha takwimu za majengo zinazoiwezesha serikali kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) Namba 11 ya mwaka 2016, ambayo yanahamasisha kufanya miji na makazi ya binadamu kuwa jumuishi, salama, himilivu na endelevu. Takwimu za sensa ya majengo pia ni muhimu katika utekelezaji wa Azimio Namba 5 la Ajenda Mpya ya Kimataifa ya Miji ya mwaka 2016, ambayo inasisitiza umakini katika kubuni, kupanga, , kufadhili, kuendeleza na kusimamia makazi ya watu hususan katika miji na majiji makubwa.

### **1.2 Malengo ya Sensa ya Majengo ya Mwaka 2022**

Lengo kuu ni kulipatia taifa takwimu za kutosha na za uhakika za majengo ili kuimarisha uamuzi unaozingatia ushahidi wa kitakwimu katika ngazi zote za utawala kwa maendeleo endelevu ya makazi ya watu.

Malengo mahususi ni kuiwezesha Serikali:

- (i) Kupata takwimu zitakazosaidia kuanzisha kanzidata ya majengo yote nchini;
- (ii) Kupitia na kuboresha sheria, kanuni, sera na mipango mbalimbali inayosimamia sekta ya maendeleo ya makazi nchini; Kupata taarifa za matumizi ya majengo mbalimbali nchini kama vile idadi ya majengo ambayo yanatumika kwa ajili ya makazi, biashara na huduma mbalimbali za kijamii zikiwemo shule, vituo vya afya, hospitali na vituo vya polisi;
- (iii) Kutathmini mchango wa Serikali katika upatikanaji wa nyumba nchini kama ilivyoelekezwa na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na Sera ya Nyumba ya Zanzibar ya mwaka 2008;
- (iv) Kutathmini kiwango cha nyumba zilizojengwa katika maeneo yaliyopangwa na yasiyopangwa; na kubaini uwiano wa upatikanaji wa huduma za kijamii katika majengo hayo; na,
- (v) Kutambua hali ya maendeleo ya miji kwa kutumia idadi ya majengo yaliyopo sasa kwa aina, kama vile majengo ya ghorofa, majengo yasiyo ya ghorofa pamoja na sifa za majengo.

## SURA YA PILI

### IDADI YA MAJENGU

#### **Matekeo Muhimu**

- Asilimia 94.4 ya majengo yote Tanzania hayana ghorofa.
- Asilimia 91.4 ya majengo yote Tanzania yanatumika kwa makazi.
- Asilimia 98.2 ya majengo yote yanayotumika kwa makazi na makazi na biashara ni ya uniti moja.

#### **2.0 Utangulizi**


Sehemu hii inatoa taarifa ya idadi ya majengo, aina ya majengo, matumizi makuu ya majengo na idadi ya uniti katika majengo ya makazi kwa ngazi ya taifa na mkoa kama ilivyobainishwa katika matokeo ya SMT 2022.

#### **2.1 Idadi ya Majengo**

Matokeo yanaonesha kuwa idadi ya majengo yote Tanzania ni 14,348,372 kati ya hayo, majengo 13,907,951 yapo Tanzania Bara na 440,421 yapo Tanzania Zanzibar. Aidha, maeneo ya vijiji yana jumla ya majengo 10,038,201 na maeneo ya mijini yana jumla ya majengo 4,310,171.

Idadi kubwa ya majengo kwa Tanzania Bara ipo katika Mkoa wa Dar es Salaam (913,707), ukifuatiwa na Mwanza (868,430) na Dodoma (836,909). Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi una idadi kubwa ya majengo (177,450) ukifuatiwa na Kaskazini Unguja (74,764) (Ramani Na.1 na Jedwali Na. 2.1).


Ramani Na. 2.1: Idadi ya Majengo kwa Mikoa; Tanzania, SMT 2022



## 2.2 Majengo yeny Anwani za Makazi


Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 74.9 ya majengo yote Tanzania yana anwani za makazi. Hali kama hiyo imeonekana pia kwa Tanzania Bara. Hata hivyo, kwa Tanzania Zanzibar asilimia 78.2 ya majengo yote yana anwani za makazi. Aidha, kwa maeneo ya vijiji asilimia 75.2 ya majengo yote yana anwani za makazi ikilinganishwa na asilimia 74.4 kwa majengo ya mjini (Kielelezo Na. 2.1 na Jedwali Na. 2.2).

Kielelezo Na. 2. 1: Mgawanyo wa Majengo (Asilimia) kwa Anwani za Makazi; Tanzania, SMT 2022



Matokeo yanaonyesha kuwa, kwa Tanzania Bara, Mkoa wa Mtwara una asilimia kubwa (88.2%) ya majengo yeny anwani za makazi ukifuatiwa na Mkoa wa Njombe (87.7%) na Kagera (83.5%). Aidha, mikoa yeny asilimia ndogo ya majengo yeny anwani za makazi ni Dodoma (63.5%), Rukwa (65.6%) na Songwe (66.2%). Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Kaskazini Pemba una asilimia kubwa ya majengo yeny anwani za makazi (89.9%) ukifuatiwa na Mkoa wa Kusini Pemba (84.5%) na Mkoa wa Mjini Magharibi ukiwa na asilimia ndogo (73.4%)(Kielelezo Na. 2.2 na Jedwali Na. 2.2).

**Kielelezo Na. 2. 2: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo yeny Anwani za Makazi kwa Mikoa; Tanzania, SMT 2022**




### 2.3 Aina za Majengo

Sensa ya Majengo Tanzania ya Mwaka 2022 imeainisha aina kuu mbili za majengo ambayo ni majengo ya ghorofa na yasiyo ya ghorofa. Matokeo yanaonesha kuwa Tanzania ina majengo mengi yasiyo ya ghorofa (94.4%) na majengo machache ya ghorofa (0.5%). Aidha, asilimia 5.1 ya majengo yote yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Asilimia ya majengo yasiyo ya ghorofa na yale ya ghorofa Tanzania Bara inawiana na ile ya Tanzania. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, asilimia 88.1 ya majengo yote siyo ya ghorofa na asilimia 1.7 ni ya ghorofa. Aidha, majengo yanayoendelea na ujenzi ni asilimia 10.2.


Matokeo pia yanaonesha kuwa asilimia 95.2 ya majengo yote vijijini siyo ya ghorofa ikilinganishwa na asilimia 92.4 kwa majengo ya mjini (Kielelezo Na. 2.3 na Jedwali Na. 2.3).

**Kielelezo Na. 2. 3: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo kwa Aina; Tanzania, SMT 2022**



Majengo mengi ya ghorofa Tanzania Bara, yapo katika Mkoa wa Dar es Salaam (3.5%) ukifuatiwa na Arusha (1.3%) na Kilimanjaro (0.7%). Aidha, Mikoa 12 ina chini ya asilimia 0.1 ya majengo ya ghorofa. Kwa Tanzania Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kuwa na majengo mengi ya ghorofa (3.1%) na mkoa wenyewe majengo machache ya ghorofa ni Kaskazini Pemba (0.3%) (Kielelezo Na. 2.4 na Jedwali Na. 2.3).

**Kielelezo Na. 2. 4: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo ya Ghorofa kwa Mkoa; Tanzania, SMT, 2022**




## 2.4 Matumizi Makuu ya Jengo

Matumizi makuu ya majengo yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni makazi, makazi na biashara na matumizi yasiyo ya makazi. Matokeo yanaonesha kuwa, majengo yanayotumika kwa makazi kwa Tanzania ni asilimia 91.4, makazi na biashara ni asilimia 3.4, na matumizi yasiyo ya makazi asilimia ni 5.2. Matumizi yasiyo ya makazi yanajumuisha majengo ya biashara, taasisi, viwanda na nyumba za ibada.

Matumizi makuu ya majengo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar yanawiana na ya Tanzania. (Kielelezo Na. 2.5. na Jedwali Na. 2.4).


Kielelezo Na. 2. 5: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo kwa Aina ya Matumizi Makuu; Tanzania, SMT 2022



Majengo yasiyo ya makazi ambayo yanatumika kwa biashara Tanzania ni asilimia 43.1 (330,302) ambapo asilimia 16.1 (126,225) yanatumika kwa shughuli za taasisi za kutoa huduma na asilimia 14.6 (111,988) ni majengo ya ibada. Hali kama hiyo ipo Tanzania Bara. Hata hivyo, majengo yasiyo ya makazi yanayotumika kwa shughuli za biashara Tanzania Zanzibar ni asilimia 35.6(8,659) wakati majengo ya Ibada ni

asilimia 25.5 (6,213) na yale yanayotumiwa na taasisi za kutolea huduma ni asilimia 14.2 (3,452) (Kielelezo Na. 2.6 na Jedwali Na. 2.5).

**Kielelezo Na. 2. 6: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo Yasiyo ya Makazi kwa Aina ya Matumizi; Tanzania, SMT 2022**




## 2.5 Idadi ya Uniti katika Jengo

Taarifa kuhusu idadi ya uniti kwenye jengo ilikusanywa kwenye majengo yanayotumika kwa makazi na kwa makazi na biashara. Matokeo yanaonesha kuwa


idadi kubwa (98.2%) ya majengo Tanzania ni yenyé uniti moja na asilimia 1.4 yana uniti mbili. Aidha, takwimu zinabainisha kuwa Tanzania ina idadi ndogo ya majengo (asilimia 0.4) yenyé uniti tatu na zaidi. Hali kama hiyo imejitokeza pia Tanzania Bara. Kwa Tanzania Zanzibar, asilimia 97.7 ni majengo ya uniti moja na asilimia 1.9 yana uniti mbili ambapo asilimia 0.4 ya majengo yana uniti tatu au zaidi (Kielelezo Na. 2.7 na Jedwali Na. 2.6).

**Kielelezo Na. 2. 7: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo ya Makazi, Makazi na Biashara kwa Idadi ya Uniti; Tanzania, SMT 2022**



Matokeo yanaonesha kuwa, zaidi ya asilimia 94.0 ya majengo ya makazi na makazi na biashara katika mikoa yote ya Tanzania yana uniti moja (Kielelezo Na. 2.8 na Jedwali Na. 2.6).

**Kielelezo Na. 2. 8: Asilimia ya Mgawanyo wa Majengo ya Makazi, Makazi na Biashara yenye Uniti Moja na Mkoa; Tanzania, SMT 2022**



Jedwali Na. 2. 1: Idadi ya Majengo kwa Aina na Mkoa; Tanzania, SMT 2022

Mkoa	Jumla				Vijijini				Mijini			
	Jumla ya Majengo	Yenye Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Ujenzi Unaendelea	Jumla ya Majengo	Yenye Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Ujenzi Unaendelea	Jumla ya Majengo	Yenye Ghorofa	Yasiyo ya Ghorofa	Ujenzi Unaendelea
Tanzania	14,348,372	68,724	13,540,363	739,285	10,038,201	11,131	9,558,456	468,614	4,310,171	57,593	3,981,907	270,671
Tanzania Bara	13,907,951	61,258	13,152,298	694,395	9,775,513	9,765	9,327,250	438,498	4,132,438	51,493	3,825,048	255,897
Dodoma	836,909	1,461	794,209	41,239	553,512	122	531,707	21,683	283,397	1,339	262,502	19,556
Arusha	553,702	7,180	515,560	30,962	369,942	1,189	347,670	21,083	183,760	5,991	167,890	9,879
Kilimanjaro	515,091	3,540	486,916	24,635	434,980	2,303	412,463	20,214	80,111	1,237	74,453	4,421
Tanga	676,397	4,282	638,604	33,511	530,746	2,514	506,135	22,097	145,651	1,768	132,469	11,414
Morogoro	762,454	1,331	724,320	36,803	496,401	277	474,759	21,365	266,053	1,054	249,561	15,438
Pwani	504,979	1,885	468,005	35,089	317,707	906	295,111	21,690	187,272	979	172,894	13,399
Dar es Salaam	913,707	32,219	827,644	53,844					913,707	32,219	827,644	53,844
Lindi	341,398	327	326,065	15,006	280,459	139	268,391	11,929	60,939	188	57,674	3,077
Mtwara	511,336	507	488,078	22,751	404,561	181	388,186	16,194	106,775	326	99,892	6,557
Ruvuma	448,328	408	434,989	12,931	359,220	181	348,852	10,187	89,108	227	86,137	2,744
Iringa	357,777	529	339,561	17,687	276,094	149	263,846	12,099	81,683	380	75,715	5,588
Mbeya	623,054	1,073	592,896	29,085	425,627	203	407,383	18,041	197,427	870	185,513	11,044
Singida	463,353	290	440,541	22,522	387,637	118	370,221	17,298	75,716	172	70,320	5,224
Tabora	680,103	400	648,178	31,525	573,378	112	550,242	23,024	106,725	288	97,936	8,501
Rukwa	302,368	173	290,707	11,488	242,894	75	234,645	8,174	59,474	98	56,062	3,314
Kigoma	458,567	318	444,481	13,768	348,054	88	338,148	9,818	110,513	230	106,333	3,950
Shinyanga	421,743	358	398,581	22,804	281,470	69	270,031	11,370	140,273	289	128,550	11,434
Kagera	716,458	701	684,987	30,770	647,291	315	620,055	26,921	69,167	386	64,932	3,849
Mwanza	868,430	2,481	801,826	64,123	588,709	164	546,814	41,731	279,721	2,317	255,012	22,392
Mara	636,185	510	595,721	39,954	459,113	176	431,424	27,513	177,072	334	164,297	12,441

Manyara	430,323	318	406,054	23,951	363,708	155	343,695	19,858	66,615	163	62,359	4,093
Njombe	279,349	322	270,529	8,498	212,301	108	206,766	5,427	67,048	214	63,763	3,071
Katavi	189,349	70	180,146	9,133	141,955	26	136,385	5,544	47,394	44	43,761	3,589
Simiyu	430,378	138	414,145	16,095	361,609	67	347,995	13,547	68,769	71	66,150	2,548
Geita	624,100	263	587,719	36,118	436,982	77	412,688	24,217	187,118	186	175,031	11,901
Songwe	362,113	174	351,836	10,103	281,163	51	273,638	7,474	80,950	123	78,198	2,629
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>440,421</b>	<b>7,466</b>	<b>388,065</b>	<b>44,890</b>	<b>262,688</b>	<b>1,366</b>	<b>231,206</b>	<b>30,116</b>	<b>177,733</b>	<b>6,100</b>	<b>156,859</b>	<b>14,774</b>
Kaskazini Unguja	74,764	466	66,676	7,622	64,179	164	57,628	6,387	10,585	302	9,048	1,235
Kusini Unguja	64,453	850	54,117	9,486	50,449	565	43,077	6,807	14,004	285	11,040	2,679
Mjini Magharibi	177,450	5,453	154,249	17,748	53,301	470	43,459	9,372	124,149	4,983	110,790	8,376
Kaskazini Pemba	63,490	222	58,280	4,988	50,571	49	46,504	4,018	12,919	173	11,776	970
Kusini Pemba	60,264	475	54,743	5,046	44,188	118	40,538	3,532	16,076	357	14,205	1,514

**Jedwali Na. 2. 2: Idadi ya Majengo kwa Anwani za Makazi kwa Mkoa; Tanzania, SMT 2022**

Mkoa	Jumla ya Majengo	Anwani za Makazi	
		Yenye Anwani za Makazi	Yasiyo na Anwani za Makazi
Tanzania	14,348,372	10,751,123	3,597,249
Vijiji	10,038,201	7,546,377	2,491,824
Mjini	4,310,171	3,204,746	1,105,425
Tanzania Bara	13,907,951	10,406,722	3,501,229
Dodoma	836,909	531,072	305,837
Arusha	553,702	410,498	143,204
Kilimanjaro	515,091	406,838	108,253
Tanga	676,397	482,127	194,270
Morogoro	762,454	536,095	226,359
Pwani	504,979	352,391	152,588
Dar es Salaam	913,707	638,673	275,034
Lindi	341,398	275,573	65,825
Mtwara	511,336	451,095	60,241
Ruvuma	448,328	370,620	77,708
Iringa	357,777	286,161	71,616
Mbeya	623,054	466,058	156,996
Singida	463,353	332,499	130,854
Tabora	680,103	482,033	198,070
Rukwa	302,368	198,424	103,944
Kigoma	458,567	353,519	105,048
Shinyanga	421,743	283,042	138,701
Kagera	716,458	598,332	118,126
Mwanza	868,430	637,231	231,199
Mara	636,185	490,774	145,411
Manyara	430,323	324,647	105,676
Njombe	279,349	244,920	34,429
Katavi	189,349	141,988	47,361
Simiyu	430,378	352,371	78,007
Geita	624,100	520,154	103,946
Songwe	362,113	239,587	122,526
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>440,421</b>	<b>344,401</b>	<b>96,020</b>
Kaskazini Unguja	74,764	56,943	17,821
Kusini Unguja	64,453	49,243	15,210
Mjini Magharibi	177,450	130,218	47,232
Kaskazini Pemba	63,490	57,058	6,432
Kusini Pemba	60,264	50,939	9,325

**Jedwali Na. 2. 3: Idadi ya Majengo ya Ghorofa kwa Idadi ya Ghorofa na Mkoa; Tanzania, SMT 2022**

Mkoa	Jumla ya Majengo ya Ghorofa	Idadi ya Ghorofa					
		1	2	3	4	5	6+
Tanzania	<b>68,724</b>	<b>53,348</b>	<b>8,587</b>	<b>3,318</b>	<b>1,485</b>	<b>752</b>	<b>1,234</b>
Vijiji	11,131	9,956	885	196	34	16	31
Mjini	57,593	43,366	7,702	3,122	1,451	736	1,203
<b>Tanzania Bara</b>	<b>61,258</b>	<b>48,296</b>	<b>6,952</b>	<b>2,803</b>	<b>1,338</b>	<b>653</b>	<b>1,191</b>
Dodoma	1,461	970	234	147	61	19	29
Arusha	7,180	6,055	687	250	90	45	52
Kilimanjaro	3,540	2,991	378	100	42	13	15
Tanga	4,282	3,840	314	81	26	7	13
Morogoro	1,331	1,042	192	63	19	6	8
Pwani	1,885	1,688	148	32	6	4	6
Dar es Salaam	32,219	24,349	3,742	1,702	974	483	967
Lindi	327	280	37	5	2	2	1
Mtwara	507	449	40	10	4	3	1
Ruvuma	408	333	45	15	4	7	2
Iringa	529	424	58	25	9	3	9
Mbeya	1,073	819	155	64	17	4	13
Singida	290	219	50	11	3	2	5
Tabora	400	304	65	16	5	2	3
Rukwa	173	136	29	6	-	0	1
Kigoma	318	272	28	10	4	3	1
Shinyanga	358	266	52	23	6	8	3
Kagera	701	578	97	15	5	1	2
Mwanza	2,481	1,776	410	161	49	34	50
Mara	510	421	54	26	3	2	2
Manyara	318	280	28	5	2	1	2
Njombe	322	273	28	16	1	1	3
Katavi	70	63	3	3	1	0	0
Simiyu	138	127	6	3	1	0	1
Geita	263	209	40	7	3	2	2
Songwe	174	132	32	7	1	1	0
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>7,466</b>	<b>5,026</b>	<b>1,635</b>	<b>515</b>	<b>147</b>	<b>99</b>	<b>43</b>
Kaskazini Unguja	466	339	91	28	6	1	1
Kusini Unguja	850	747	81	14	5	2	0
Mjini Magharibi	5,453	3,455	1,359	400	111	88	40
Kaskazini Pemba	222	178	28	9	7	0	0
Kusini Pemba	475	307	76	64	18	8	2

**Jedwali Na. 2. 4: Idadi ya Majengo kwa Aina Kuu ya Matumizi na Mkoa; Tanzania, SMT 2022**

Mkoa	Jumla ya Majengo	Matumizi Makuu		
		Makazi	Makazi na Biashara	Yasiyo ya Makazi
Tanzania	<b>14,348,372</b>	<b>13,112,235</b>	<b>493,093</b>	<b>743,044</b>
Vijiji	10,038,201	9,307,250	242,259	488,692
Mjini	4,310,171	3,804,985	250,834	254,352
<b>Tanzania Bara</b>	<b>13,907,951</b>	<b>12,717,893</b>	<b>470,476</b>	<b>719,582</b>
Dodoma	836,909	769,832	25,219	41,858
Arusha	553,702	491,037	25,817	36,848
Kilimanjaro	515,091	460,586	22,066	32,439
Tanga	676,397	616,127	25,824	34,446
Morogoro	762,454	700,295	29,223	32,936
Pwani	504,979	458,160	21,462	25,357
Dar es Salaam	913,707	786,485	74,466	52,756
Lindi	341,398	319,177	7,625	14,596
MtWARA	511,336	477,590	8,789	24,957
Ruvuma	448,328	416,127	12,883	19,318
Iringa	357,777	320,991	11,161	25,625
Mbeya	623,054	563,569	18,845	40,640
Singida	463,353	422,658	13,091	27,604
Tabora	680,103	634,671	16,209	29,223
Rukwa	302,368	281,736	9,584	11,048
Kigoma	458,567	429,031	7,317	22,219
Shinyanga	421,743	387,927	14,763	19,053
Kagera	716,458	658,982	22,635	34,841
Mwanza	868,430	812,432	21,958	34,040
Mara	636,185	593,634	14,701	27,850
Manyara	430,323	384,972	18,829	26,522
Njombe	279,349	246,759	8,881	23,709
Katavi	189,349	173,903	5,698	9,748
Simiyu	430,378	399,564	10,312	20,502
Geita	624,100	585,017	14,366	24,717
Songwe	362,113	326,631	8,752	26,730
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>440,421</b>	<b>394,342</b>	<b>22,617</b>	<b>23,462</b>
Kaskazini Unguja	74,764	67,943	3,011	3,810
Kusini Unguja	64,453	58,097	2,618	3,738
Mjini Magharibi	177,450	156,267	12,789	8,394
Kaskazini Pemba	63,490	57,519	2,260	3,711
Kusini Pemba	60,264	54,516	1,939	3,809

**Jedwali Na. 2. 5: Idadi ya Majengo Yasiyo ya Makazi kwa Aina ya Matumizi na Mkoa; Tanzania, SMT 2022**

Mkoa	Ofisi	Biahsara	Viwanda	Nyumba za watalii	Nyumba za kulala Wageni	Hoteli	Maghala	Taasisi	Mabalozi / Mashirika ya Kimatatifa	Taasisi za Kidini	Viwanda Vidogo vidogo
Tanzania	58,484	330,302	10,851	1,674	24,029	12,454	54,207	126,225	626	111,988	34,849
Vijijiini	30,913	213,456	5,718	1,134	9,252	6,404	41,998	82,736	388	82,152	24,584
Mjini	27,571	116,846	5,133	540	14,777	6,050	12,209	43,489	238	29,836	10,265
Tanzania Bara	56,321	321,643	10,496	1,422	23,456	11,683	52,927	122,773	538	105,775	34,337
Dodoma	2,896	19,054	698	11	1,107	472	2,935	6,563	21	6,718	2,194
Arusha	3,289	16,944	499	486	1,418	1,327	2,497	6,646	21	4,280	1,625
Kilimanjaro	2,708	16,667	532	96	656	539	1,469	6,112	31	3,574	1,362
Tanga	2,601	13,186	508	63	887	880	1,524	6,505	17	7,572	1,738
Morogoro	2,621	13,455	564	61	1,303	431	2,505	5,758	26	5,127	1,943
Pwani	2,303	11,427	453	69	689	416	1,035	4,568	17	4,056	847
Dar es Salaam	6,645	27,890	1,056	64	2,312	942	2,563	7,060	55	5,630	1,567
Lindi	1,285	6,531	174	20	299	127	750	3,171	13	1,735	702
Mtware	2,035	14,229	202	4	281	193	1,254	3,658	12	2,603	900
Ruvuma	1,955	6,380	500	12	487	165	1,335	4,439	18	3,132	1,551
Iringa	1,973	12,815	407	112	637	218	1,147	4,088	16	3,541	1,452
Mbeya	3,154	19,487	615	50	1,156	493	2,604	5,428	36	6,813	1,939
Singida	1,687	12,208	448	11	572	323	2,400	4,440	23	4,543	1,549
Tabora	1,832	11,005	448	10	995	313	4,696	4,871	12	3,932	1,727
Rukwa	908	3,412	191	16	396	99	659	2,228	9	2,657	762
Kigoma	1,541	11,109	137	21	566	299	1,189	3,735	19	3,204	812
Shinyanga	1,530	7,142	440	8	1,042	405	1,402	3,765	23	2,810	1,169
Kagera	2,257	17,160	247	22	741	449	1,997	5,185	30	6,688	815
Mwanza	2,623	13,574	493	30	2,094	845	2,923	6,904	23	4,263	1,612
Mara	1,911	11,002	333	52	1,292	932	2,130	5,958	19	3,497	1,630
Manyara	1,656	9,616	202	106	605	462	3,163	4,588	23	5,597	1,196

Njombe	2,097	12,422	361	18	571	171	927	3,324	16	3,262	1,137
Katavi	573	4,569	203	23	471	137	826	1,417	1	1,108	640
Simiyu	1,003	6,623	196	36	719	365	5,233	3,930	17	1,881	1,030
Geita	1,604	10,034	293	14	1,606	466	2,238	4,967	21	3,170	927
Songwe	1,634	13,702	296	7	554	214	1,526	3,465	19	4,382	1,511
<b>Tanzania Zanzibar</b>	<b>2,163</b>	<b>8,659</b>	<b>355</b>	<b>252</b>	<b>573</b>	<b>771</b>	<b>1,280</b>	<b>3,452</b>	<b>88</b>	<b>6,213</b>	<b>512</b>
Kaskazini Unguja	298	1,397	52	121	216	267	148	471	12	945	69
Kusini Unguja	302	1,237	66	77	209	269	160	520	21	924	84
Mjini Magharibi	967	3,707	133	33	89	146	607	1,236	24	1,618	211
Kaskazini Pemba	285	1,080	46	15	19	39	227	620	19	1,373	55
Kusini Pemba	311	1,238	58	6	40	50	138	605	12	1,353	93

**Jedwali Na. 2. 6: Idadi ya Majengo ya Makazi, Biashara na Makazi kwa Idadi ya Uniti na Mkoa; Tanzania, SMT 2022**

Mkoa	Idadi ya Majengo	Idadi ya Uniti									
		1	2	3	4	5	6	7	8	9	10 na zaidi
Tanzania	13,496,202	13,254,160	189,936.	30,966.00	10,432.00	3,583	2,631	908	1,027	425	2,134
Vijiji	9,462,837	9,366,375	79,422	11,739	3,089	965	618	175	137	58	259
Mjini	4,033,365	3,887,785	110,514	19,227	7,343	2,618	2,013	733	890	367	1,875
<b>Tanzania Bara</b>	<b>13,077,844</b>	<b>12,845,485</b>	<b>181,916</b>	<b>30,015</b>	<b>10,093</b>	<b>3,485</b>	<b>2,549</b>	<b>887</b>	<b>990</b>	<b>415</b>	<b>2,009</b>
Dodoma	793,108	780,766	9,814	1,620	469	153	148	35	23	11	69
Arusha	524,154	510,927	9,788	1,863	774	292	194	58	84	24	150
Kilimanjaro	493,992	482,544	9,152	1,374	511	141	112	45	30	21	62
Tanga	638,599	627,095	9,785	1,060	393	94	89	16	14	9	44
Morogoro	711,551	697,068	11,782	1,713	530	170	125	42	42	11	68
Pwani	446,046	437,330	6,979	1,153	329	107	67	25	17	12	27
Dar es Salaam	866,020	813,984	36,553	7,789	3,197	1,247	992	364	538	220	1,136
Lindi	327,521	325,252	1,874	268	65	22	22	1	4	2	11
Mtwara	500,995	496,068	4,182	485	152	37	31	9	17	0	14
Ruvuma	436,292	430,614	4,778	610	196	45	23	11	6	2	7
Iringa	348,367	342,640	4,909	527	146	59	47	6	9	2	22
Mbeya	593,314	582,093	9,327	1,220	342	121	96	32	31	12	40
